KISWAHILI BIDHAA ADIMU: JIAJIRI



Elizabeth Godwin Mahenge

© Elizabeth Godwin Mahenge

Chapa ya Kwanza 2011

Picha ya kwenye gamba imepakuliwa kutoka kwenye wavuti wa Tanzanaiti http://www.google.co.tz/search?q=tanzanite

DIBAJI

Kitabu hiki kinachambua nafasi ya Kiswahili kama kitega uchumi. Je, bidhaa hii inawezaje kumkomboa na kumtajirisha Mswahili? Jibu la swali hili ni kwamba, kwa kutafsiri kazi mbalimbali zilizoandikwa kwa lugha nyinginezo – kunaweza kumpa soko la ajira mzungumzaji wa Kiswahili. Zipo fursa mbalimbali ambazo zitamwezesha mzungumzaji wa lugha hii kuondokana na umaskini wa kipato. Kitabu hiki kitabainisha kinagaubaga namna ya kutajirika kwa kupitia lugha ya Kiswahili. Fursa kadha wa kadha zitaelezwa kinagaubaga ili kuwezesha soko la ajira kwa kutumia Kiswahili.

Kitabu hiki kitatumia nadharia ya lugha kama bidhaa kama inavyotajwa na Bourdieu (1977, 1982, na 1991) kama alivyonukuliwa katika Simmons 2000. Pia tutatumia nadharia ya 'thamani' ambayo inaangalia uzuri wa vitu asilia – yaani uzuri wa lugha ya Kiswahili kuwa bidhaa.

Katika nadharia hizi, watu wanaelewa thamani ya lugha yao pamoja na lugha nyinginezo ambazo zinatumika katika mazingira yao. Kwa kuzingatia hilo, watu wanafanya uamuzi (uchaguzi) wa kujua lugha gani na kutumia lugha gani katika mazingira husika www.lingref.com/cpp/wss/1/paper1003.pdf. Kwa maneno mengine, nadharia hizi zinaangalia hadhi ya lugha katika maswala ya kiuchumi – je, mtu ajifunze lugha

gani na kwa nini. Hapa ndipo suala la uchaguzi au uamuzi wa kujua au kufahamu lugha fulani unapojitokeza.

Kitabu hiki itakuwa na sura tatu ambazo ni utangulizi, kiini, na hitimisho. Katika utangulizi tutagusia usuli kuhusu lugha ya Kiswahili ikiwemo nini maana ya ‘uadimu’ wa bidhaa hii ya Kiswahil pamoja na muktadha wa lugha hii katika ulimwengu wa utandawazi. Katika kiini tutazungumzia nadharia za ubidhaishaji na thamani ya Kiswahili pamoja na fursa mbalimbali za kukibidhaisha Kiswahili. Katika sehemu ya hitimisho, tutatoa mapendekezo ya nini kifanyike ili Watanzania waweze kushindana katika dunia hii ya ushindani bila kujitenga au kutengwa.

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Kiswahili ni miongoni mwa lugha kumi za dunia zikiwemo Kiingereza na Kifaransa (Chachage, h.t). Kiswahili kwa sasa kinasemwa katika dunia nzima, hii ni kutokana na ukweli kwamba, mataifa mengi duniani yanakazana ama kuanzisha kozi zinazofundisha Kiswahili au kufungua vyombo vya habari kama vile: magazeti, majarida, redio na televisheni. Kwa hali hii, Kiswahili kitasambaa duniani kote kwa kasi ya ajabu ndani ya muda mfupi ujao. Hili ni jambo la faraja kwa wadau na wapenzi wa lugha hii ya Kiswahili.

Juhudi mbalimbali zinaendelea kufanywa kitaifa na kimataifa ili kukiwezesha Kiswahili kisambae kila mahali ambako kinauwezo wa kufika. Jambo hili litawezekana kutokana na ukweli kwamba, tayari Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje Mheshimiwa Bernard Membe – amefungua Kituo cha Kufundishia Kiswahili katika makao makuu ya Umoja wa Afrika tarehe 26/1/2012. Habari hii imeandikwa na Assah Mwambene kutoka Addis Ababa Ethiopia http//:www.issamichuzi.blogspot.com/.../hon-membe-launched-first-kiswahili.ht.

Si hivyo tu, bali juhudi nyingine zimeshafanywa za kuunda Chama cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani

(CHAUKIDU) Chama hii kitakuwa na makao yake makuu katika mji anamoishi na kufanya kazi Rais wa chama, na kwa sasa ni katika Chuo Kikuu cha Wisconsin-Madison, Marekani. Madhumuni makuu ya Chama cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani (CHAUKIDU) ni: Kuwajumuisha pamoja waendelezaji wa Kiswahili duniani kote kwa lengo la kuchochea kasi ya kukuza Kiswahili; kusambaza habari na matokeo ya utafiti; kushauri ama kushinikiza serikali za nchi ambamo Kiswahili kinazungumzwa kutambua thamani iliyobebwa na maliasili hii ili kuunda sera muafaka za kukiendeleza kadri ya uwezo wake kwa manufaa ya maendeleo ya serikali na watu wake kijamii, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni; kujumuisha pamoja wanachama kwa ajili ya kubadilishana mawazo na tajiriba zao katika masuala mbalimbali yanayohusu Kiswahili; na kusambaza habari na matokeo ya utafiti kwa kutumia kijarida, jarida, na teknolojia ya mtandao wa kompyuta juu ya vipengele mbalimbali vya Kiswahili na masuala yanayohusiana na Kiswahili (Che-Mponda, 2012).

1.0.1 MUKTADHA WA KITABU

Muktadha wa bidhaa hii ni katika ulimwengu wa kiutandawazi na kileberali mamboleo ambao unaangalia kila kitu kupitia fedha na faida. Kuiangalia lugha kama bidhaa ambapo itaweza

kuleta fedha na faida. Ulimwengu wa kileberali tunaweza kuutazama katika nchi ya Tanzania tangu kuchipuka kwa SAP (*Structural Adjustment Policy*) ambapo watu walitakiwa wachangie ili kupata huduma za msingi na ukawa ndio mwisho wa kupata huduma za bure. Katika muktadha huo, waliokwama wanataka kujikwamua ili waondokana na umaskini unaowakabili; ni sauti ya tabaka la kati ambalo ni la wasomi na ni la watu wa uwezo wa kati (sio maskini na wala sio matajiri).

1.0.2 KUADIMIKA KWA KISWAHILI

Nini maana ya kuadimika kwa Kiswahili: je kipo ila ni kwa wachache; je kinahitaji ‘wavunaji’ wengi; au je ni sitiari ya Kibiblia ya kwamba, mavuno ni mengi ila watendakazi ni wachache? Maswali mawili ya mwisho yana msingi katika hoja tutakazozitoa katika kitabu hiki. Kiswahili ni bidhaa ‘adimu’ kwa sababu kinahitaji ‘wavunaji’ wengi zaidi kwa kuwa, waliopo hawatoshi. Vilevile, sitiari ya Kibiblia pia inatufaa katika kitabu hiki kwa kuwa, kuna soko kubwa sana la bidhaa hii ya Kiswahili lakini watendaji ambao wamekubali kujitosa kwenye uuzaji wa bidhaa hii bado ni wachache sana.

1.0.3 SULA LA KINADHARIA

1.0.3.1 Nadharia ya thamani kwa mkabala wa kiuchumi

Ni nadharia ya sayansi ya jamii ambayo inachambua kuhusu uzalishaji, usambazaji, na matumizi ya vitu na huduma. Neno uchumi linatokana na neno la Kigiriki *oikonomia* ambalo linamaanisha 'kudhibiti nyumba na kutawala' na *oikos* maana yake 'nyumba'+ *nomos* 'desturi' au 'sheria', hivyo 'kanuni, sheria na desturi za kutawala nyumba' http://en.wikipedia.org/wiki/Value_theory. Labda tunaweza kuiboresha maana hiyo na kusema 'kanuni za kutawala soko au kanuni za kudhibiti soko' kwa kuwa dhana ya nyumba si mahsusi zaidi kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili; ila maana ya awali katika Kigiriki ilikuwa hivyo – yaani udhibiti wa nyumba au kutawala nyumba. Kwa hiyo, kwa muktadha wetu ni kudhibiti soko la Kiswahili.

Nadharia ya kukipa kitu thamani au kukithamini kitu inahusisha mikabala mbalimbali inayowezesha kuelewa ni kwa vipi, kwa nini, na kwa kiwango gani watu wanathamini vitu; kama vitu hivyo ni watu, mawazo, vifaa, au kitu chochote kile. Utafiti na uchunguzi huu ulianzia kwenye filosofia ya kale liyoitwa akziolojia (yaani nadharia ya thamani) au maadili. Uchunguzi wa kale wa kifalsafa ulijikita katika kuchunguza wema na ubaya na dhana ya 'uzuri'. Hivi leo nadharia ya thamani au uthamani ni ya kisayansi zaidi, ikichunguza watu wanathamini nini na kwa nini wanathamini vitu hivyo katika miktadha mbalimbali kama vile kisaikolojia, kijamii, na kiuchumi. Mkabala tutakaoufuata katika natharia hii ya thamani ni ule wa kiuchumi http://en.wikipedia.org/wiki/Value_theory

Kwa ujumla wake, kuna tofauti kati ya uzuri wa kimaadili na uzuri wa vitu asilia. Uzuri wa kimaadili ni kwa yale mambo yanayohusisha roho au matendo ya mtu. Hasahasa kusifia na kulaumu. Uzuri wa vitu asilia kwa upande mwingine, unashughulikia vitu, na sio watu. Kwa mfano, ukisema *'Maria ni mtu mzuri'* inaweza kuhusisha hisia tofauti za dhana ya 'uzuri' kuliko ukisema *'oh, chakula hii ni kizuri'* http://en.wikipedia.org/wiki/Value_theory

Maadili yanajikita kwenye uzuri wa kiroho na kimatendo kuliko uzuri wa vitu asilia; wakati uchumi unajihusisha na kinyume chake yaani inaangalia uzuri wa vitu na sio matendo ya mtu (utu). Hata hivyo, aina zote za uzuri – yaani uzuri wa kiroho (au kimaadili na kimatendo) na uzuri wa vitu asilia – aina zote hizi za uzuri zina umuhimu katika nadharia ya uzuri na thamani ambayo ni pana sana http://en.wikipedia.org/wiki/Value_theory

Umuhimu wa kuitumia nadharia hii unatokana na mada yetu tunayoishughulikia katika kitabu chetu kuwa na mwelekeo huo wa kibidhaa. Tunaangalia soko la lugha – yaani lugha kama bidhaa ambayo inapelekwa sokoni kuuzwa na kununuliwa. Hivyo katika nadharia hii, tunaichukua lugha ya Kiswahili kama bidhaa na kuipa thamani ambapo tunaangalia uzuri kwa mkabala wa pili – yaani uzuri wa vitu asilia. Nadharia hii ya uthamani wa kiuchumi inatupeleka kwenye vipengele vya 'kanuni, sheria au maadili ya kudhibiti na kutawala soko'. Soko likiwa ni lugha ya Kiswahili – kwamba ni kwa vipi watu wanaithamini, kwa nini wanaithamini, na kwa kiwango gani wanaithamini. Katika kuichambua hoja hii, tutatumia mawazo ya wachambuzi mbalimbali ambao wamechambua lugha kama bidhaa ya kupelekwa sokoni. Mawazo yao tutayaona katika sehemu inayofuatia hapa chini.

1.0.3.2 NADHARIA YA LUGHA KAMA BIDHAA

Bidhaa ni istilahi inayotumika kumaanisha kitu chochote kinachoweza kuuzika ambacho kimetengenezwa ili kutosheleza mahitaji ya watu. Bidhaa za kiuchumi zinaweza kuwa ni kitu au huduma http://en.wikipedia.org/wiki/Commodity. Zipo tafiti mbalimbali ambazo zimekwishafanywa kuhusiana na jambo hili kama vile Rubdy R, na Tan, P (2008), Simmons (2000), na Heller (2010) kwa kuwataja kwa uchache. Kwa mfano, Heller anazungumzia maeneo sita ambayo yanatumika katika kubidhaisha lugha na kuifanya iwe bidhaa inayouzwa na kununuliwa. Maeneo hayo ni kama vile: utalii, masoko na matangazo, ufundishaji wa lugha, tafsiri, vituo vya mawasiliano kama simu na kompyuta, na sanaa za maonesho www.annualreviews.org/doi/abs/10.../annurev.anthro.012809.10495.

Mtu mwingine ambaye amechambua mawazo ya Pierre Bourdieu kuhusu Kitabu yake ya *Linguistic Market and Linguistic Capital* kwamba, ni msomaji wa maswala ya kijamii wa Chuo Kikuu cha Liverpool. Msomaji huyu anaelezea soko la lugha analolimaanisha Bourdieu ni ule uwezo alionao mtu wa kuzungumza moja kwa moja kwenya hoja, kwa namna

ambayo inakidhi muktadha na malengo ya mazungumzo hayo. Ni uwezo wa kutumia maneno sahihi, sarufi sahihi, rejista, kiimbo, au lugha ya ishara na kadharika kwa namna ambayo inakubalika katika muundo wa soko la bidhaa hii ya lugha (Jumapili, Novemba 12, 2011). Soko la lugha kama jina lenyewe linavyojionesha, linajengwa kwenye uhusiano wa kiuchumi ambapo, kuna watu wana uwezo mkubwa wa kiisimu au kilugha katika matumizi ya lugha husika na kuna watumiaji ambao uwezo wao ni mdogo, hicho ndicho kitu ambacho Bourdieu anakizungumzia.

Msomaji huyo anaelezea kuwa, ili kufahamu soko hili la lugha linalozungumziwa, hebu fikiria jinsi Oxford wanavyotumia Kiingereza na kumpa mzungumza lugha sahihi ya kutumia, ambayo ni rasmi, Kiingereza chao kina mamlaka na kinampa mzungumzaji hadhi fulani kuliko Kiingereza cha mtu mweusi. Hii inajidhihirisha kupitia katika matumizi ya lugha ambayo yanampa hadhi mtu fulani anayezungumza Kiingereza kizuri ikilinganishwa na yule anayezungumza Kiingereza kibovu.

Kwa msisitizo tutadondoa hapa ujumbe huo ili ieleweke kuwa kauli hiyo hapo juu sio yangu mwandishi wa kitabu hiki. Dondoo ni kama ifuatavyo:

> To understand Bourdieu's idea of the linguistic market and linguistic capital, think about how Oxford English gives a speaker, in formal situation, much more voice and credibility than someone who speaks, for example, Black English. This is determined by the formation of the linguistic market which gives certain ways of communication a more favorable currency in comparison with others… http://culturalstudiesnow.blogspot.kr/2011/11/pierre-bourdieus-concept-of-linguistic.html

Kwa hiyo, kinachoelezwa na mwandishi huyo japo kinaweza kuonekana kina dharau ndani yake – hasa anaposema 'Kiingereza cha mtu mweusi', tunaweza kuitumia kauli hiyohiyo tukizungumzia Kiswahili. Kwamba, ili kulielewa wazo la soko la lugha, tunaweza kufikiria ni kwa vipi TUKI/TATAKI na Tanzania inampa mzungumzaji Kiswahili kizuri, ambacho ni rasmi, chenye mamlaka, na kinachompa hadhi mzungumzaji ambaye anakitumia, ikilinganishwa na Kiswahili kibovu kinachozungumzwa na mzungu.

Jambo hili linajidhihirisha kupitia katika matumizi sahihi ya lugha ambayo yanampa hadhi mtu fulani anayezungumza Kiswahili kizuri ikilinganishwa na yule anayezungumza Kiswahili kibovu. Kwa hiyo, kutokana na hoja hiyo tuliyoidondoa hapo juu, kitu kinachofuatia katika sehemu ya pili ya kitabu hiki ni kuonesha sasa, mavuno hayo yatokanayo na bidhaa ya lugha yako wapi?

SURA YA PILI

KIINI

2.0 MAVUNO YAKO WAPI?

Katika kulijibu swali hili la mavuno yako wapi – tutawasilisha hoja mbalimbali ambazo zinaonesha kuwa ni kwa vipi lugha ya Kiswahili ni mtaji katika soko hili la lugha. Kwa kuwa, tunakichukua Kiswahili kuwa ni bidhaa: kwa mantiki kwamba, tunaweza kukiuza Kiswahili na watu wengine wanaweza kukinunua – basi hatuna budi kuonesha ni kwa vipi lugha hii ni bidhaa.

Kwanza, kwa kufanya kazi ya kutafsiri kazi mbalimbali zilizoandikwa kwa lugha nyinginezo na kuzipeleka katika Kiswahili au kinyume chake – kunaweza kumpa soko la ajira mzungumzaji wa Kiswahili. Hoja hii ya tafsiri kama njia mojawapo ya kubidhaisha lugha inaelezwa pia na Heller (2010) katika makala yake iitwayo *The "Commodification of Language"* www.annualreviews.org/doi/abs/10.../annurev.anthro.012809.10495.

Hili litawezekana endapo wahusika watachangamka na kuzitafuta kazi hizi kwa kufanya mawasiliano na wahusika. Mathalani, katika nchi yetu kuna mashirika mbalimbali ya kimataifa ambayo yanafanya kazi zao nchini mwetu: mashirika

haya ya kigeni yanafanya shughuli zao kwa lugha zao za kigeni – hivyo, hapa kuna ajira au tuite soko kwa kuwa, wanahitaji kuhawilisha taarifa zao kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa.

Inabidi mzungumzaji wa lugha hii ambaye pia ana ujuzi wa kutafsiri afanye mawasiliano na ofisi hizi ili kuona kama kuna kazi ya kuhawilisha maarifa kutoka lugha moja na kwenda lugha nyingine. Hili litawezekana kwa Waswahili hawa kusoma na kupata ujuzi wa kutafsiri au kukarimani.

Lakini sio tu kusubiri kazi za kutafsiri kutoka katika makampuni au ofisi za kigeni tuu, mfasiri anapaswa kuwa mjasiriamali kwa kutafuta vitabu mbalimbali ambavyo anaona maarifa yake yanaweza kupata soko na kuvitafsiri vitabu hivyo. Kwa mfano, kama kuna kitabu cha saikolojia na kimeandikwa kwa lugha ya kigeni – na unajua fika kuwa, somo hilo ni muhimu kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na vyuo vya ualimu – basi unakitafsiri kitabu (kwa kuomba ruhusa kutoka kwenye kampuni ya uchapishaji); kisha unakuwa umejipatia ajira. Kitabu kitanunuliwa na kusomwa na wewe utaweza kujiajiri na kuwaajiri watu wengine. Hiyo ni fursa mojawapo.

Pili, kama anavyoeleza Mahenge (2011) katika kitabu cha *Sanaa ya Uigizaji: Waigizaji na Waongozaji wa Filamu,*

Michezo ya Kuigiza ya redioni, Tv, na Jukwaani anasema kwamba, Watanzania wanaweza kujiajiri kupitia maeneo matatu ambayo ni: sanaa, soka, na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa wageni. Katika upande wa sanaa, anawafumbua macho Watanzania kuwa, sanaa ya uigizaji ni taaluma, hivyo, anawashauri Watanzania wakasomee taaluma hiyo katika vyuo vya sanaa ndani na nje ya nchi ili wapate ujuzi na kujiajiri katika sanaa ya uigizaji. Kwa kufanya hivyo, wasanii wa Tanzania wataweza kutengeneza kazi bora za kisanaa na kupata masoko.

Katika kipengele hii cha sanaa, anazungumzia pia wanamuziki – ambao wanaweza kutengeneza santuri zao za miziki ya Kiswahili (kwa Kiswahili na kwa lugha zetu za asili) na hivyo kuziuza santuri zao kwenye soko la dunia. Wanamuziki hawa wanatakiwa wachangamkie soko hili na kuziuza kazi zao ndani na nje ya nchi. Kwa kufanya hivyo, miziki yao ya Kiswahili na ya Kitanzania itapata soko na hivyo watajiajiri.

Katika hoja ya soka, anapongeza hatua ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dokta Jakaya Kikwete kwa kurudisha tena michezo mashuleni (UMITASHUNTA), ambayo ilifutwa na aliyekuwa Waziri wa Elimu Bwana Joseph Mungai. Katika mashindano hayo ya UMITASHUNTA, vipaji

vya michezo vilikuwa vikinolewa na watoto wa Watanzania waliweza kujiajiri kupitia tasnia hiyo. Jambo hili lilipunguza tatizo la kukosekana ajira kwa vijana: kwa kuwa, wengi wao walijiajiri katika michezo (Mahenge, 2011). Hiyo ni fursa nyingine ya kujipatia soko la ajira kupitia katika michezo huku utambulisho wa watu hawa ukiwa ni lugha ya Kiswahili na nchi ya Tanzania.

Kitu cha mwisho anachokizungumzia Mahenge katika kitabu hicho ni ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa wageni (wasiokijua Kiswahili). Hoja hii pia inaelezwa na Heller (2010) katika makala yake ya ubidhaishaji wa lugha. Mahenge (2011:4) anaeleza jambo hili kama ifuatavyo:

> Watanzania wamejaliwa na Mwenyezi Mungu kwa rasilimali za kila aina na Kiswahili kikiwemo. Kiswahili ni ajira kama zilivyo ajira za lugha nyinginezo kama vile: Kiingereza, Kifaransa kwa kuzitaja kwa uchache. Watanzania tuamke kuchangamkia ajira za kufundisha Kiswahili - sio lazima kwenda nje ya nchi. La! Ajira hizi tunaweza kuzifanyia hapa nyumbani kwa kuwa kila kukicha wageni wanakuja Tanzania na wanashauku ya kujifunza lugha na utamaduni wa Mtanzania. Hii inawezekana kwakuwa, wanafunzi wanaosomea shahada mbalimbali za elimu hapa nchini huku wakichukua Somo la Kiswahili kama somo la kufundishia – waanzishe madarasa ya kufundisha Kiswahili kwa wageni. Wanaweza kuanzisha kitu kinachoitwa 'SWAHILI CLASSES FOR BIGINNERS' - madarasa haya hayana budi kuanzishwa ili tuweze kuwapatia ajira Watanzania wenzetu ambao wana ujuzi mbalimbali kuhusiana na utamaduni wa Mtanzania. Ujuzi kama mapishi, utengenezaji wa batiki, uchezaji ngoma za asili na zile za ubunifu, na mambo kadha wa kadha ambayo Watanzania

wamejaaliwa na Mwenyezi Mungu hapa duniani.

Jambo hili linawezekana kwa kuwa: nguvu tunazo, uwezo tunao, na nia tunayo. Hii itawezekana tu kama wanafunzi hawa watatumia vizuri ujuzi huo wa Isimu ya Kiswahili yaani fonolojia, sintaksia, mofolojia, pragmatiki, leksikografia, na semantiki - wataweza kufundisha mada hizo huku wakishirikiana na watu wengine ambao watafundisha vitu vingine ambavyo sio vya kiufundi kuhusiana na ujifunzaji wa lugha.

Katika kulitekeleza hili, tunaiomba Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi isaidie kusimamie jambo hili ili wababaishaji wasipotoshe fursa hii. Wahakikishe walimu

Nne, tufungue kampuni zetu za uchapishaji ambazo zitachapisha vitabu vilivyoandikwa kwa Kiswahili kwa wingi. Vitabu hivi viwe ni vya kufundisha taaluma mbalimbali pamoja na vya burudani kama vile kazi za fasihi – vitabu vya ushairi, hadithi fupi, riwaya, na tamthiliya. Vitabu vya kufundishia Kiswahili vichapishwe kwa wingi kwa kulenga soko mahususi – yaani kufundisha Kiswahili kwa wale wasiokijua kabisa (wageni). Kwa kufanya hivyo, kutakuwa na machapisho mengi ambayo yakiuzwa yanawawezesha Watanzania kupata fedha na hivyo kuzidi kusonga mbele – bidhaa ikiwa ni Kiswahili. Uchapishaji usiishie hapo, bali

juhudi za kuyatangaza machapisho haya iwepo kupitia mitandao ya kijamii na mitandao ya wanataaluma. Pia kupeleka machapisho hayo katika semina na makongamano mbalimbali ambayo yanafanyika ndani na nje ya nchi. Katika miktadha hiyo, vitabu vinanunuliwa kwa wingi na hiyo tayari ni ajira. Kuna watu kazi yao ni kusambaza vitabu, kuviuza, kuviandika, kuvichapisha na kadharika. Mbona ndani ya kifungu hii kuna fursa kadha wa kadha?

Tano, kama nchi yetu itaunda sheria ya kukimudu Kiswahili (kwa ambao sio Watanzania ambao wanataka kuja kufanya kazi Tanzania) kabla ya kufika Tanzania – itawezesha ajira kwa Watanzania. Kwa vipi? Hili litawezekana kama serikali itafungua vituo mbalimbali vya kufundisha Kiswahili katika kila nchi duniani ambako, wafanyakazi wanaotaka kuja Tanzania kufanya kazi kama wakandarasi, wawekezaji, wafanyabiashara na kadharika – watasoma Kiswahili japo kwa miezi mitatu na kufanya mtihani wa kuandika na kuzungumza. Mwanafunzi huyu wa Kiswahili akifaulu anapewa cheti na kinakuwa ni kigezo namba moja cha kuja kufanya kazi au kuishi katika nchi ya Tanzania.

Jambo hili linawezekana ni kama ambavyo wenzetu wanaoheshimu na kuzienzi lugha zao wanavyofanya – yaani wanakutaka ufanye mtihani wa Kiingereza kabla hujaenda

ughaibuni (nazungumzia mitihani ya TOEFL) na kadharika. Kwa nini na sisi tusiringie Kiswahili chetu? Kwanini kusiwe na mtihani kabla mgeni hajaja kuishi Tanzania? Kwa nini tusiwe na kitu tutakachokiita **JAKUKI** kwa maana ya ***Jaribio la kupima kumudu kuzungumza na kuandika Kiswahili.*** Hiyo 'KU' moja itatumika kumaanisha 'kupima kumudu, kuzungumza na kuandika. 'KU' zingine tumezidondosha kutokana na sababu za uikisadi. Hili linawezekana na ni njia mojawapo ya Watanzania kutajirika na bidhaa hii adimu ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia.

Sita, ukarimani nalo ni eneo ambalo linawezesha kutengeneza ajira. Mathalani, Watanzania wakiamua kujifunza lugha mbalimbali ambazo ni kubwa duniani – kama vile Kiingereza, Kijerumani, Kichina kwa kuzitaja kwa uchache – itawawezesha kujiajiri kwa kuwa, watakarimani kwenye mikutano ya kimataifa kutoka lugha hizo na kwenda katika Kiswahili. Hii ni ajira kwa hiyo Watanzania wajifunze kuchangamka na kuzitafuta fursa kama hizi kwa kwenda vyuoni kujifunza fani hii ya ukarimani. Ukishapata ujuzi hakuna mtu ataweza kukupokonya: ni wewe tu utatakiwa sasa kuutumia ujuzi wako kujiajiri.

Saba, lugha ya kufundishia katika shule zetu tangu ngazi ya chekechea hadi chuo kikuu iwe ni Kiswahili. Hoja hii ni

muhimu kwa kuwa, watu wetu wataweza kuyapata maarifa kwa kutumia lugha wanayoielewa. Hivyo wataweza kutumia akili zao na utashi wao ili kubuni na kugundua vitu. Tunaweza kujiuliza ni nani katika dunia hii ambaye anatumia lugha asiyoielewa na akaweza kugundua kitu kipya? Sidhani kama nitapata jibu la kuridhisha katika swali hili – lakini ni ukweli usiopingika kuwa, ukiwa unajifunza kitu kwa lugha unayoijua, basi unapata fursa ya kuitumia akili na ubunifu wako katika kuleta gunduzi mbalimbali.

Hoja hii vilevile ni muhimu katika suala la uchumi wa nchi yetu na kwa kukitumia Kiswahili katika kufundishia, itawezesha kupata pesa ambazo zimekuwa zikitumwa nje ya nchi kununulia vitabu vilivyoandikwa kwa Kiingereza – zitabakia hapahapa nchini kwa kununua vitabu ambavyo vimeandikwa kwa Kiswahili. Kwa kufanya hivyo, soko letu la vitabu litakuwa na uchumi utapanda. Kwani watu wengi watakuwa na ajira binafsi na za kuajiriwa kutokana na kuifanya lugha ya kufundishia kuwa ni Kiswahili.

Nane, tukope hoja za Heller (2010) zinayohusu utalii, vituo vya mawasiliano, pamoja na masoko na matangazo kama njia mojawapo ya kubidhaisha lugha na tuijadili katika muktadha wetu wa Kiswahili. Lugha ya Kiswahili inaweza kubidhaishwa kupitia utalii kwa sababu, watalii wengi wanatembelea nchi

yetu kwa lengo la burudani na kujipumzisha. Tumeshuhudia kila mwaka msimu wa baridi kali huko Ulaya na Marekani na sehemu nyinginezo duniani – ambapo, watalii wanakuja Afrika ya Mashariki na hasa Tanzania ili kuona wanyama, mbuga, na rasilimali chungu nzima zilizopo.

Katika muktadha huo, wanakuja pia kujifunza lugha na tamaduni za watu waishio katika maeneo hayo yenye vivutio. Kwa hiyo, sekta ya utalii inaongeza pato la taifa na vilevile inatengeneza ajira – kwani wahudumu wa hoteli na wasindikizaji mbugani wanahitajika ili kumwezesha mtalii afurahie neema iliyopo hapa Tanzania. Hii ni fursa ya ajira kwa kuwa kupitia utalii huo, tutaweza kutangaza utamaduni wetu wa Kitanzania. Hili linawezekana kama zitatengenezwa santuri zinazoelezea tamaduni za Watanzania na utalii uliopo na kisha zikauzwa. Kwa kufanya hivyo, tayari kuna soko la ajira kupitia utalii.

Tisa, vituo vya mawasiliano kama simu na mitandao ya kompyuta nayo inahusika katika kubidhaisha lugha. Vituo hivi vinahusisha vyombo vya habari ambavyo hupata taarifa na kuzisambaza kwa walaji (Heller, 2010). Vyombo hivi vya habari kama vile redio, televisheni, magazeti, na intaneti – vyote kwa pamoja vinaweza kutumika kutengeneza ajira za watu. Ajira hizi ni kupitia lugha ya Kiswahili. Mathalani,

tukiwa na vituo vya utangazaji vinavyotangaza kwa Kiswahili – je hatujatengeneza ajira? Au tukiwa na magazeti yanayoandikwa kwa Kiswahili – je hatujatengeneza ajira? Kwa hakika, kupitia katika hoja hii ya vituo vya mawasiliano, tunaweza kutengeneza ajira chungu nzima kwa kukitumia Kiswahili kwa ajili ya Watanzania.

Kumi, masoko na matangazo nayo ni njia mojawapo ya kubidhaisha lugha (Heller, 2010). Katika eneo hili, lugha inapata masoko kupitia matangazo mbalimbali kama vile utengenezaji wa bidhaa ambazo zimeandikwa maneno kwa lugha ya Kiswahili. Mathalani, inawezekana kutengeneza fulana zenye maandishi ya Kiswahili na kupitia maandishi hayo kukapatikana soko la bidhaa hiyo. Si fulana pekee, bali hata khanga zetu zinazotengenezwa hapa nchini nazo kupitia maandishi yake ambayo yako kwa Kiswahili – yanaweza kuwa ni kivutio kikubwa sana na hivyo kukapatikana soko la Kiswahili kupitia khanga.

Namna tulivyoifafanua hoja hii ni tofauti na alivyoieleza Heller kwani yeye ameegemea kwenye utengenezaji wa ajira hasa kwa wanawake kama vile wahudumu, wake, na watumishi wa ndani. Sisi tumeegemea katika masoko na matangazo ya bidhaa kwa kutumia Kiswahili. Kwani huu ni ukweli usiopingika, kila mwaka wakija wageni hapa Tanzania,

wanavutiwa na maandishi ya kwenye khanga zetu na hivyo wanazinunua khanga hizi. Sio kwamba wanavutiwa na khanga, la, wanavutiwa na maneno. Huu ni ushahidi ambao ninao kutokana na uzoefu wa kuwafundisha Wazungu, Wamarekani, Wachina na Waingereza ambao wamekuwa wakija Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kujifunza Kiswahili tangu mwaka 2002 hadi 2010 nilipokuwa mwanafunzi wa shahada ya kwanza na ya pili.

Kumi na moja ni kufungua wavuti na blogi ambazo Watanzania wanazitumia katika kutangaza bidhaa hii kwa wateja wao. Tunajua fika kuwa, wateja wa bidhaa hii ni wale wasioijua – kwa hiyo, ili kuwafikia ni kwa kutengeneza matangazo na kuyarusha kwenye njia mbalimbali za mawasiliano ikiwemo magazeti, redio, televisheni, tovuti, wavuti, na blogi. Sambamba na hili ni kujua namna ya kuwasiliana na wateja hawa - ili bidhaa iweze kuuzika barabara.

2.1 Hadhi ya Kiswahili

Kama ambavyo Moshi (2011) alivyoelezea kwenye Kitabu yake ya The Globalized world Language: the Case of Kiswahili amedadavua ni kwa vipi sasa hivi katika karne hii ya 21,

Kiswahili kimekuwa lugha ya utandawazi. Ameelezea sababu mbalimbali kama vile: matumizi ya lugha hii ya Kiswahili kama lugha rasmi, lugha ya taifa, au lugha ya mawasiliano mapana katika nchi mbalimbali za Afrika Mashariki. Pia ametaja suala la matumizi ya Kiswahili katika shughuli za kiserikali na kibiashara; kiuchumi na kiutamaduni. Pia ameelezea jinsi Kiswahili kinavyofundishwa kwa kasi katika sehemu mbalimbali za dunia ikiwemo Marekani, Ulaya na Bara Asia. Vilevile, amezungumzia redio za kimataifa ambazo zinatumia Kiswahili katika matangazo yake ikiwemo DW, VOA, BBC, na nyinginezo nyingi.

Si hivyo tu, katika Kitabu hayo amezungumzia jinsi Bill Gates mwaka 2004 mwezi wa Julai alivyoamua kuiingiza lugha ya Kiswahili katika programu ya kompyuta ya Maikrosofti. Yote haya ni maandalizi ya kuiwezesha lugha ya Kiswahili kutandawazika na kusambaa duniani kote. Amezungumzia makampuni ya simu kama vile Vodacom na Airtel ambayo nayo yameingiza lugha ya Kiswahili katika matangazo yao ili waweze kuwapata wateja mbalimbali kulingana na lugha za mawasiliano wanazozitumia. Pia alizungumzia ujasiri wa Rais wa Msumbiji Joakimu Chisano ambaye katika mkutano wa Umoja wa Afrika, aliamua kimatendo kuzungumza Kiswahili na hiyo ikawa ni hatua

sahihi ya kuiwezesha lugha hii kuingia katika matumizi ya lugha za Umoja wa Afrika (Moshi, 2011:170).

Kwa muhtasari, hiyo ndiyo hadhi ya lugha ya Kiswahili duniani kama ilivyoelezewa katika Kitabu ya Moshi.

SURA YA TATU

3.0 HITIMISHO

Ninaposisitiza ajira binafsi kwa Watanzania ya kukiuza Kiswahili - simaanishi kwamba Watanzania wasijifunze lugha nyinginezo za kigeni kama vile Kiingereza, Kifaransa, Kispaniola, Kijerumani, Kiarabu, Kichina na kadharika kwa kuzitaja kwa uchache.

Ni muhimu Watanzania tuzijue lugha hizo ili tuweze kuwasiliana nao 'hao wanafunzi' ambao watakuwa wanajifunza Kiswahili chetu. Na kufunzwa huku Kiingereza hakuna budi kufanywa kwa usahihi - tunaiomba serikali ikubali kugharamia Watanzania ambao watakwenda kwenye nchi za kigeni kujifunza lugha za wenzetu kwa umahiri na kisha waje watufundishe sisi wengine ambao ama hatukijui Kiingereza na lugha nyinginezo au tunakijua cha kukiboronga.

Vilevile, serikali ichukue hatua ya kugharamia walimu wageni ambao watakuja Tanzania kukifundisha Kiingereza na lugha nyingine za kigeni kwa ufasaha. Hii ni kwa kukifundisha Kiingereza au lugha za kigeni kwa **kutumia mbinu za kumfundisha mgeni lugha ya pili** na sio kumkaririsha mwanafunzi sarufi ya lugha husika: hapa ninamaanisha muhtasari '*syllabus'* kwa kimombo. Muhtasari wa kufundisha somo la Kiingereza ubadilishwe ili ulenge kumwezesha

mwanafunzi kumudu kuzungumza (kwani uliopo sasa unasisitiza kujua sarufi ya lugha. Hoja hii imezungumzwa sana na watafiti kama vile Martha Qorro na F.E.M.K Senkoro wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam). Mbinu hizi zipo na ndio maana wageni wanapokuja kujifunza Kiswahili hapa Tanzania - hasa Idara ya Kiswahili iliyopo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wanatumia wiki moja tu na mwanafunzi huyu mgeni anakuwa na umahiri wa kuwasiliana na Watanzania *'angalau kile cha kuombea maji'*. Na baada ya wiki mbili, mwanafunzi huyu mgeni anabwabwaja Kiswahili tena kwa ufasaha na vilevile kile cha mitaani - utafikiri alizaliwa nacho. Sasa iweje Watanzania washindwe kubwabwaja Kiingereza na lugha nyinginezo? Haya yanawezekana kwa kuifundisha lugha ya Kiingereza na lugha nyinginezo za kigeni kwa misingi ya ufundishaji wa lugha ya pili.

Si hivyo tu, bali ufundishaji wa taaluma mbalimbali au ujuzi mbalimbali ufanywe kwa lugha ambayo Watanzania wanaielewa. Hapa simaanishi lugha za makabila-lahasha! Namaanisha lugha ya Kiswahili. Lugha hii ina hadhi sawa na lugha zinginezo zinazotumika katika ufundishaji. Tatizo ni utashi wa kisiasa tu. Nguvu hii ya kukiwezesha Kiswahili kushika hatamu hizo ni pamoja na kuingizwa katika Katiba ya nchi yetu (Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) ili mambo haya

yaende kisheria. Jambo hili la kuingiza Kiswahili katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia limejadiliwa katika Kitabu ya Mulokozi (2005). Tunaendelea kusisitiza kuwa, lugha ya kufundishia katika vyuo vya umma iwe ni Kiswahili na lugha za kigeni kama Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani, na kadharika - zifundishwe kwa misingi ya ufundishaji wa lugha ya pili kwa mgeni. Lugha ya Kiingereza itumike kufundishia katika vyuo vya binafsi na vile vya kimataifa - ambavyo vitapenda kuchukua wanafunzi wa kutoka sehemu mbalimbali za dunia kama vifanyavyo vyuo vikuu sehemu mbalimbali duniani mfano Ujerumani, Korea, China, Norway, Finland, Italy na Australia kwa kuvitaja kwa uchache. Ili ifike wakati, Watanzania wawe ni mahiri kwa lugha zaidi ya tano hadi sita - hili linawezekana kwa kuwa Watanzania ni binadamu sawa na binadamu wengine.

Suala la ufundishaji kwa kutumia Kiswahili limejadiliwa sana na watafiti kama vile F.E.M.K Senkoro na M. Qorro lakini matokeo ya tafiti zao yamepuuzwa. Kwahiyo hakuna hoja ya msingi inayohalalisha 'wengine wazijue lugha nyingi za kigeni ambazo wanajifunza' na Watanzania wasizijue – HAKUNA! Watanzania wana uwezo wa kushindana na watu wengine duniani kote kwa hiyo serikali ichukue hatua ya kutuwezesha ili tusijitenge au tusitengwe na dunia.

Ninaposisitiza ufundishwa wa maarifa, taaluma, na elimu kwa kutumia Kiswahili – siko vitani na Kiingereza. Naomba nieleweke vema. Kuna baadhi ya watu wanapotosha harakati hizi kwa makusudi! Hao wana lao jambo. Mimi sina ugomvi na Kiingereza. Tena nataka Watanzania wasijue Kiingereza tu – bali wajue zaidi ya lugha tano za kimataifa ili wawe walumbi kwelikweli.

Mwisho, nitamalizia kitabu changu kwa kutoa shukrani za dhati kwa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukiunga mkono Kiswahili. Ili kuthibitsha jambo hili nitaweka nukuu mbili: moja ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano Dkt. Jakaya Kiwete; na ya pili itakuwa ni ya Mheshimiwa Waziri wetu Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. “Lugha ya Kiswahili imeanza kupata umaarufu Afrika na duniani. Umoja wa Afrika umekubali Kiswahili kuwa moja ya lugha zake kuu. Aidha, nchi za Kanda ya Maziwa Makuu zimekubali kutumia na kuendeleza Kiswahili. Serikali yenu ya awamu hii itahakikisha kuwa juhudi hizi zinaendelezwa na kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inakua nje ya mipaka ya Afrika” (mwaka 2005).

Kauli ya pili ni hii hapa: “Mheshimiwa Spika, katika mkutano huu wa Bunge letu, waheshimiwa wabunge walipokea na kujadili pamoja na mambo mengine maazimio mbalimbali.

Niruhusu nirejelee Azimio lililonigusa sana kuhusu Uanzishaji wa Kamisheni ya Lugha ya Kiswahili. Awali, BAKITA na CHAKITA na wawakilishi kutoka Uganda walianzisha wazo la kuwa na mpango wa kuundwa kwa Baraza la Kiswahili la Afrika Mashariki. Hata hivyo, Baraza hilo halikuanzishwa, badala yake ikapendekezwa kuanzisha Kamisheni ya Lugha ya Kiswahili. Azimio la Kuanzishwa kwa Kamisheni hiyo ya Lugha ya Kiswahili tumelipitisha katika Bunge hili. Nitumie fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri sana mliyoitoa" (mwaka 2012).

Marejeo

Che – Mponda, C. *Chama cha Ukuzaji Kiswahili Duniani.* (2012). *swahilitime.blogspot.com/.../chama- cha-ukuzaji-w.*

Heller, *M. The Commodification of Language* Annual Review of Anthropology. Vol. 39: 101-114 (Volume publication date October 2010)**http://www.annualreviews.org/doi/full/10.1146/annurev.anthro.012809.104951**

Mahenge, E. *Sanaa ya Uigizaji: Waigizaji na Waongozaji wa Filamu, Michezo ya Kuigiza ya redioni, Tv, na Jukwaani,* (2011)http://www.lulu.com

_____, *Kiswahili Bidhaa Adimu: Jiajiri.* (2012). n.p. Dar es Salaam

_____, *Kiswahili Kama Silaha ya Ukombozi wa Bara la Afrika: Ukombozi wa Kiuchumi. (*2012). TUKI: Dar es Salaam

Mwambene, A. *"Hon. Membe lauched the First Kiswahili Class at the Language Center of the African Union".* (2012) *issamichuzi.blogspot.com/.../hon-membe-launched-first-kiswahili.ht...*

Reader, University of Liverpool, *culturalstudiesnow.blogspot.com, (2011),* http://culturalstudiesnow.blogspot.kr/2011/11/pierre-bourdieus-concept-of-linguistic.html

Rubdy R, na Tan, P. *Language as Commodity: Global Structures, Local Marketplaces ☐ Continuum.* (2008) International Publishing Group Ltd. London.

Simmons, M. Language Shift and Linguistic Markets in Barcelona.
(2000).www.lingref.com/cpp/wss/1/paper1003.pdf